# *BARUA #02; JINSI YA KUPATA HAMASA ISIYOISHA.*

Kwako rafiki yangu mpendwa,

Umehudhuria semina na kupata mafunzo mazuri, umehamasika sana na kuondoka ukiwa na nguvu ya kwenda kufanya mabadiliko makubwa kwenye maisha yako. Unaanza kutumia hamasa hiyo kuleta mabadiliko kwenye maisha yako lakini siku chache baadaye hamasa hiyo inaisha na unarudi kwenye maisha yako ya kawaida.

Umesoma kitabu au kusikia ushuhuda wa mtu akielezea jinsi alivyotoka chini kabisa na kufanikiwa. Unaona kama yeye aliweza hata wewe unaweza pia. Unaondoka ukiwa na hamasa kubwa, unaenda kuchukua hatua ulizojifunza kwa mtu huyo, lakini haikuchukui muda hamasa hiyo inazima na unarudi kwenye mazoea.

Kila mmoja wetu amewahi kupitia hali hizi, hata mimi mwenyewe, kuna wakati nasoma au kuandika kitu, kinanihamasisha mwenyewe na kusema kuna hatua za tofauti nitakwenda kuchukua, nachukua hatua hizo kwa siku chache lakini siendelei tena.

## Tatizo ni nini?

Kwa kuwa kila mtu anapitia hali hii, ni vyema tukajua tatizo ni nini ili kama tunataka kutoka hapo, tujue njia sahihi ya kuondokana na hali hiyo.

Jamii imekimbilia kusema tatizo ni hamasa, pita mitandaoni na utaona jinsi kuna utani mwingi juu ya wahamasishaji, wakionekana kama ni matapeli, ambapo wanatumia mifano au hadithi za uongo kuwahamasisha wengine.

Kuna kichekesho huwa nakiona mtandaoni kinasema; tumetoka kumpiga motovational speaker hapa, ambaye ametuambia alianza na unyoya wa kuku na sasa kafikia kuku elfu moja.

Utani wa aina hii ni mwingi lakini ujumbe ulio nyuma ya utani huu ni kwamba tatizo la hamasa kutokudumu ni wahamasishaji ambao wanatumia hadithi zisizo kweli au zisizowezekana.

Lakini jibu haliwezi kuwa rahisi hivyo, kwa sababu hata kwenye maisha yako ya kawaida tu, kuna mtu unamjua, ambaye unajua kwa namna yoyote ile umemzidi kwenye vitu vingi, iwe ni elimu, umri, koneksheni na hata rasilimali lakini ameweza kupiga hatua kubwa kuliko ambazo wewe umepiga.

Hivyo tatizo ni zaidi ya hamasa.

## Njiti ya kiberiti.

Ukiwa na kuni, mkaa au gesi, unajua kabisa vina nguvu ya kukuwezesha kupika chakula. Lakini ukiweka sufuria juu ya jiko ambalo halijawaka, hata usubiri kwa muda mrefu kiasi gani, hakitaiva.

Tunajua kiberiti kina nguvu ya kuanzisha moto, lakini hata ukinunua maboksi mengi kiasi gani

ya viberiti, huwezi kutumia moto wa kiberiti kupika chakula kikaiva.

Hebu fikiria unawasha kila njiti na kutegemea chakula kiive, hata kama una njiti nyingi kiasi gani, huwezi kuivisha chakula.

Hapa tumeona vitu viwili, kuni/mkaa/gesi ambavyo vina nguvu kubwa ya kuivisha chakula, lakini mpaka vianzishwe na tuna kiberiti ambacho kinaweza kuanzisha moto, lakini moto huo pekee hauwezi kuivisha chakula, mpaka ukutane na kuni/mkaa/gesi.

Hivi ndivyo uhusiano wa hamasa na wewe ulivyo.

Hamasa ni njiti ya kiberiti na wewe ndiye kuni/mkaa/gesi. Hamasa inaanzisha moto ambao unatakiwa uendelee kuchochewa na wewe.

Hebu niambie, ukiwasha kiberiti halafu kuni zisishike moto, utalaumu kiberiti? Jibu ni hapana, kama njiti imewaka lakini kuni

hazikuwaka, basi tatizo lipo kwenye kuni, labda ni mbichi au kuna tatizo jingine.

Hivyo inapokuja kwenye hamasa na wewe, haijalishi hamasa ni ya aina gani, kama pale mwanzoni ulipata msukumo fulani na kuanza kuchukua hatua, baadaye hamasa hiyo ikapotea, tatizo siyo hamasa, **TATIZO NI WEWE.**

Tatizo ni wewe kushindwa kutumia hamasa uliyoipata kuwasha moto mkubwa ndani yako. Hivyo unaendelea kuhangaika na njiti zaidi kitu ambacho hakisaidii, kwa sababu kama tulivyoona, njiti pekee haziwezi kuivisha chakula.

Kama unataka kufikia mafanikio makubwa kwa kutegemea hamasa za nje tu, huna tofauti na anayetaka kupika makande kwa kutumia moto wa njiti za kiberiti pekee. Kwa kifupi haiwezekani.

Kwenye barua ya leo kwako rafiki yangu, nakwenda kukushirikisha jinsi unavyoweza kutengeneza hamasa itakayodumu na

kukuwezesha kuchukua hatua kubwa na kufanikiwa kwenye maisha yako.

## Anzia ndani.

Kama tulivyoona, tatizo kubwa la hamasa linaanzia ndani ya mtu, hivyo ili kupata hamasa inayodumu, hatua ya kwanza ni kuanzia ndani yako.

Lazima wewe mwenyewe uwe na msukumo ambao umelala, ambao hamasa ya nje inakwenda kuanzisha na kazi yako inakuwa kuuchochea kila siku ili uweze kufanya makubwa.

Lazima ndani yako uwe na maono makubwa, uwe na picha ambayo unaiona na unataka kuifikia, na hapo ndipo utaweza kutumia hamasa ya nje kuchukua hatua.

Kwa kifupi kabisa, hatua ya kwanza na ya muhimu ya kupata hamasa isiyoisha ni KUJUA KWA HAKIKA NINI UNACHOTAKA. Lazima ujue, bila ya shaka yoyote na bila ya kubahatisha ni

nini unachotaka kupata au kufikia kwenye maisha yako.

Kama hujui unachotaka hata ungepewa hamasa na nani, haiwezi kukusaidia kabisa.

Chukua mfano mzuri kwa wale ambao kila mara wanahangaika na fursa mpya. Leo kasikia ushuhuda wa mtu akielezea kuhusu matikiti, aliweka milioni mbili kwenye heka moja, baada ya miezi mitatu kavuna milioni 12. Kesho yake anatoka na kwenda kuanza kilimo cha matikiti. Anaweka milioni zake mbili, baada ya miezi mitatu anavuna laki saba.

Hajafikiria nini kimetokea kwenye hayo matikiti, anasikia ushuhuda wa mfugaji wa kuku, aliyeanza na kuku kumi, baada ya mwaka amefikia zaidi ya kuku elfu moja, anauza mayai, vifaranga na kuku wenyewe. Anatoka mbio na kwenda kununua vifaranga wa kuku, na wala hataki kuanza na vifaranga kumi kama mwenzake, atachelewa, anaanza na vifaranga 100, miezi miwili baadaye vifaranga wote wamekufa.

Naweza kuendelea na mifano hii, lakini picha unayo, mtu atajikuta mahali pa miaka michache amejaribu fursa zaidi ya kumi na zote ameangukia pua. Atakimbilia kusema wahamasishaji wamemdanganya, lakini hawezi kukaa chini na kujiuliza swali hili rahisi; NI NINI HASA NINACHOTAKA KWENYE MAISHA YANGU?

Bila kujibu swali hilo, hakuna atakachoweza kufanya.

Kwenye mwongozo wetu wa MWAKA WA MAFANIKIO 2020/2021 hili lilikuwa swali la msingi ambalo kila mtu alipaswa kulijibu, ipi ndoto kubwa ya maisha yako, unajiona ukiwa wapi.

Unaweza kuliona ni swali rahisi, lakini lina uzito mkubwa mno ndani yake, ni swali litakalokuwezesha kutengeneza hamasa ya kudumu na itakayokuwezesha kufanya makubwa na kufanikia kwenye maisha yako.

# KWA NINI UTESEKE?

Umeshajua wapi unataka kufika, hongera, umekamilisha asilimia 1 ya safari yako. Sasa mbele yako kuna asilimia 99 ya safari, ambayo bado hujaianza.

Wote tunajua kabisa kwamba kila kitu kwenye maisha kina gharama, na kadiri kitu kilivyo na dhamani kubwa, ndivyo gharama yake inakuwa kubwa.

Hivyo kila ndoto uliyonayo, ina gharama ambayo unapaswa kuilipa. Kama ndoto ni kubwa, gharama ya kulipa ni kubwa zaidi.

Baada ya kujua NINI HASA UNACHOTAKA, hatua ya pili itakayokusaidia kupata hamasa inayodumu ni kujua KWA NINI UTESEKE.

Iko wazi kwamba safari ya mafanikio haitakuwa rahisi. Ndiyo utasikia kuna watu wameweka milioni mbili wakavuna milioni kumi na mbili, lakini hiyo siyo mara yao ya kwanza kujaribu hivyo. Walishapitia kupoteza kwingi, wakajifunza mengi kwa mateso mpaka wakafika kwenye kuvuna kiasi hicho.

Lakini wewe unataka uvune mazuri ya mwisho bila kulipa gharama, lazima utakuwa unachekesha.

Kuna gharama ya kulipa, kuna mateso utakayokutana nayo, kama huna sababu kwa nini uteseke, hutafika mbali.

Kwa kila unachochagua, kuna njia mbili zitajitokeza mbele yako, njia ya kwanza ni rahisi, ambayo inakupa manufaa kidogo sasa lakini inakuzuia usipate manufaa makubwa baadaye. Na njia ya pili ni ngumu, ambayo inakupa mateso sasa, lakini baadaye inakupa manufaa makubwa.

Nini kitakufanya uiache njia rahisi na kwenda kwenye njia ngumu?

Kwa sababu hilo ni kwenda kinyume kabisa na asili ya binadamu, ni sawa na kutegemea maji yapande mlima. Kila binadamu akipewa njia mbili, rahisi na ngumu, atachagua rahisi, siyo udhaifu wako, ni asili yako.

Ndiyo maana hii dunia ina watu wachache sana waliofikia mafanikio makubwa, kwa sababu hao ndiyo waliokuwa na moyo mgumu, wa kuacha kilicho rahisi sasa na kufanya kilicho kigumu.

Hebu fikiria, una ajira ambayo inakulipa vizuri sana, ambapo unaendesha maisha yako vizuri, lakini inakubana kiasi cha kukosa muda wa kufanya vitu vingine. Unakutana na fursa ambayo umekuwa unaifuatilia, lakini ili kuifanya inabidi uache kazi yako. Kila mtu anakujua kwa kazi hiyo, umepanda ngazi na kufika vyeo vya juu, ni nani aliye na uthubutu wa kuacha kitu cha uhakika na kwenda kuanza kitu ambacho hana uhakika nacho?

Hapo ndipo utengano wa wanaofanikiwa sana na wanaobaki kawaida unapoanzia, utayari wa kuacha njia rahisi na kukabili njia ngumu.

Aliyekuwa mwanafalsafa wa ujerumani, Friedrick Nietzche aliwahi kunukuliwa akisema; Yule mwenye KWA NINI KUBWA, yuko tayari kukabiliana na ugumu wowote ule utakaojitokeza mbele yake.

Ni kutoka kwenye kauli hiyo ya Nietzche ndipo tunapata msingi wa pili wa kujijengea hamasa idumuyo, KWA NINI NITESEKE.

Kwa chochote kile ulichochagua kufanya, lazima ujue gharama unayopaswa kulipa, lazima ujue mateso unayokwenda kukabiliana nayo kisha kujua kwa nini utakuwa tayari kuteseka.

Lazima uwe na sababu ya kuacha njia rahisi inayokuja mbele yako na kuchagua njia ngumu, kitu ambacho siyo asili yako kabisa.

Hapa nakwenda kukushirikisha KWA NINI tano ambazo zimetumiwa na wengi, unaweza kuchagua kati ya hizi au ukatengeneza ya kwako. Muhimu ni uwe na kitu kinachokupa nguvu ya kuendelea na safari yako bila kukata tamaa.

## KWA NINI TANO UNAZOWEZA KUTUMIA.

Hapa nakwenda kukushirikisha KWA NINI tano ambazo zimetumiwa na wengi, na jinsi unavyoweza kuzitumia wewe pia. Lakini pia

utakuwa huru kutengeneza kwa nini yako kulingana na kile unachotaka.

## Kwa nini ya kwanza; kusudi la maisha.

Umelijua kusudi la maisha yako na umeamua kulitimiza, hivyo uko tayari kuteseka kwa sababu maisha yako hayatakuwa na maana kama hutafikia ndoto uliyoichagua.

Hii ni kwa nini yenye nguvu kwa sababu inaanzia ndani yako na inasukumwa zaidi na upendo ulio ndani yako na uimara wako pia.

Kwa nini hii haihitaji ubadili chochote, bali inahitaji uchague kuwa wewe na utoe mchango kwenye maisha kupitia ndoto yako.

Kwa nini hii inakusukuma kwa sababu haupo tayari kuishi maisha ya aina nyingine, haijawahi kukutokea ukajiona unaishi maisha tofauti na ndoto uliyoichagua. Ni kitu ambacho kipo ndani yako na unakifanya kwa sababu ndiyo maisha yako.

**Jinsi ya kutumia kwa nini hii;** jua kusudi la maisha yako, kupitia vitu ambavyo unapenda

kuvifanya au kuvifuatilia, kisha jipe jina la vitu hivyo. Ukishajipa jina, utahitaji kulitimiza. Mfano kama unapenda kuandika na umechagua uandishi kuwa ndoto yako, jiite mwandishi. Sasa huwezi kujiita mwandishi ambaye huandiki. Kila unachofanya, jione ukiwa mtu ambaye ameshafanikiwa kwenye kitu hicho na maisha yako yanaelezewa kwa kitu hicho. Iwe ni mwalimu, daktari, mfanyabiashara, mhamasishaji na mengine, yafanye maisha yako kuwa kitu hicho na hilo litakusukuma kufanya bila ya kuchoka au kuacha.

## Kwa nini ya pili; kupata uhuru kamili.

Kila tunachofanya kwenye maisha, ni kwa sababu tunataka vitu vikuu viwili; FURAHA na UHURU. Hakuna kingine tunachotafuta kwenye haya maisha, ni hivyo viwili tu.

Lakini kwa wengi imekuwa kama mtego, kila ambacho mtu anafanya ili kupata vitu hivyo viwili, anazidi kuvipoteza. Mfano mtu anatumia kilevi ili apate furaha, kilevi kinapoisha furaha aliyoipata anaikosa, lakini pia anakuwa ameleta uchovu na kujisikia vibaya ambapo kunamfanya

azidi kukosa furaha. Mtu anayetaka kupata uhuru wa muda wake anaweza kujituma sana kwenye kazi au biashara yake ili apate kipato kikubwa, lakini kufanya hivyo kunamfanya awe na majukumu zaidi yanayozidi kubana muda wake.

Hivyo kwa nini ya pili na yenye nguvu ambayo unaweza kuitumia kupata hamasa isiyokuwa na ukomo ni kutaka kupata UHURU KAMILI. Hapa unazungumzia kuwa na uhuru wa kufanya kile unachotaka, wakati unaotaka na watu unaowataka wewe. Kwa kifupi hulazimiki kufanya chochote ambacho hutaki.

Uhuru kamili una gharama kubwa na kwa kuwa ni kitu kizuri kinachokufanya uishi maisha yako utakavyo, ni kwa nini unayoweza kuitumia.

Jinsi ya kutumia kwa nini hii; jua uhuru kamili wa maisha yako ni nini, hasa kwenye kiwango cha fedha unachopaswa kuwa nacho kama akiba, uwekezaji na faida inayozalishwa kwenye uwekezaji. Kisha tumia picha ya kufikia uhuru

kamili kama kitu cha kukusukuma kuendelea na safari yako hata kama umechoka kiasi gani.

## Kwa nini ya tatu; kuwasaidia wengine.

Chochote unachofanya, kuna namna kinawagusa wengine. Hata kama unafanya ili unufaike wewe, bado ni wengine ndiyo watakaokunufaisha. Hivyo unaweza kuwatumia hao wengine kama kwa nini ya kukusukuma wewe uendelee kufanya.

Kwa kazi au biashara unayoifanya, waangalie wale ambao unawasaidia, ambao kama usingekuwepo wewe, hata kama wana fedha, wasingepata kile kinachowanufaisha.

Ona tofauti unayoileta kwenye maisha ya wengine, ambapo ukiacha kufanya, watu hao watakosa kitu kikubwa na maisha yao yatakuwa hovyo sana.

Kisha tumia hicho kama msukumo kwako kuendelea kufanya. Ona ni wajibu wako na kama hutafanya, siyo tu unajinyima mwenyewe, bali pia unawadhulumu wengine.

Kama hutatengeneza unachotengeneza, kama hutatekeleza majukumu yako, kuna wengine watateseka, hivyo wewe ndiye wa kulaumiwa. Ukijiweka kwenye nafasi hii, utapata msukumo wa kuendelea, kwa sababu unaona umuhimu wa kile unachofanya.

**Jinsi ya kutumia kwa nini hii;** kwa kile unachofanya, iwe ni kazi au biashara, angalia wale wanaonufaika na matokeo unayozalisha, angalia jinsi matokeo yako yanavyobadili maisha yao, kisha fanya huo kuwa wajibu wako. Ona ukiacha kufanya, unavyowaangusha wengi wanaotegemea kile unachofanya na hapo utasukumwa kuendelea kufanya.

## Kwa nini ya nne; kuacha jina zuri.

Mwandishi mmoja amewahi kusema, kila tunachofanya ni kujaribu kukiepuka kifo. Wale wanaohangaika kufanya mambo yanayoacha alama, ni kutaka majina yao yaendelee kuwepo hata watakapokufa. Na hakuna ubaya kwenye hilo, iwapo utakumbukwa kwa yaliyo mema.

Julius Nyerere, Nelson Mandela, Reginald Mengi, Hendry Ford, Thomas Edison na wengine wengi ni watu ambao hawapo hai sasa, lakini majina yao yanaishi nasi kila siku. Tunawakumbuka kwa mambo mbalimbali waliyofanya walipokuwa hai na yakaacha alama kubwa ambayo inaendelea kuishi mpaka sasa.

Unaweza kutumia hili kama kwa nini ya wewe kuteseka, kwa kuchagua kufanya kitu ambacho kitaacha kumbukumbu kwa vizazi vijavyo. Unajua kabisa kwa hayo majina niliyotaja hapo juu kuna wengi ambao walikuwa nao karibu, lakini leo hatuwajui, kwa sababu walichagua maisha ya kawaida, ya raha ya haraka. Lakini hao niliowataja, wote kwa nyakati tofauti, walichagua njia ngumu, Nyerere kwa kupingana na wakoloni, Mandela kwa kufungwa jela miaka 27, yote hayo yalikuwa magumu kwao, lakini hawakuyakimbia, na leo hii tunawakumbuka.

**Jinsi ya kutumia kwa nini hii;** angalia ni sifa gani unayotaka kuiacha ikiishi hapa duniani hata utakapokufa, kisha itumie kukusukuma kuchukua hatua sahihi kila siku. Kila unapojikuta

unashawishika kufanya kilicho rahisi, jikumbushe lengo lako ni kuacha alama na alama huachwa kwa kufanya magumu na makubwa.

## Kwa nini ya tano; kuwaonesha wengine unaweza/inawezekana.

Kuna watu wengi huwa wanafanikiwa kwa hasira, kwa sababu waliambiwa hawawezi kabisa na wakabisha wakisema wataweza. Ahadi waliyoitoa kwa wengine kwamba wataweza, inawasukuma kufanya makubwa zaidi. Kwa sababu wanajua kama wakishindwa, watachekwa na wale waliowaambia hawawezi. Kwa nini hii huwa ina msukumo mkubwa, hasa pale inapokutana na hasira kubwa.

Kuna watu ambao wametokea mazingira ambayo wengi wanaamini haiwezekani, lakini wao wanaona kama kwa wengine imewezekana, hata kwao pia inawezekana. Lakini wakiwaambia watu bado hawaamini. Hivyo wanachagua kufanya na wafanikiwe, ili kuwaonesha wengine inawezekana na kuwapa

hamasa na wao ya kuchukua hatua. Hii ni kwa nini yenye nguvu pia, hasa unapotaka kuwa sehemu ya mabadiliko ya jamii.

**Jinsi ya kutumia kwa nini hii;** kumbuka mtu yeyote ambaye amewahi kukuambia hutaweza kufanikiwa kwenye maisha na jiambie unakwenda kumwaibisha kwa mafanikio makubwa utakayoyapata na kila unapotaka hamasa ya kufanya zaidi, pata picha ya mtu huyo akiwa anakucheka, hapo utapata msukumo zaidi. Pia angalia jamii iliyo nyuma yako, ambayo imekata tamaa na kuamini mambo hayawezekani, chagua kuwa sehemu ya tumaini lao, ukijua kushindwa kwako kutawakatisha tamaa zaidi na kufanikiwa kwako kutawapa moyo nao wachukue hatua, chagua kufanikiwa ili uwape moyo.

Hizi ni kwa nini tano ambazo zimekuwa zinatumiwa na wengi na zimewapa msukumo makubwa na unaodumu maisha yao yote. Lakini kama nilivyokueleza, unaweza kutengeneza kwa nini nyingine yoyote ile, muhimu ni iweze kukupa hamasa na msukumo wa kuendelea

kuchukua hatua hasa pale unapokutana na magumu yanayowapelekea wengine kukimbia.

## KWA NINI YAKO NI IPI?

Umejifunza kwa kina jinsi ya kutengeneza hamasa inayodumu kwa KUJUA UNACHOTAKA na KWA NINI UTESEKE.

Kwenye majibu uliyotuma kwenye email ulieleza NINI UNACHOTAKA, sasa rudi kwenye email ile ile na ongeza jibu la swali hili; KWA NINI UTESEKE?

Eleza ndoto yako kuu na kisha ongeza maelezo hayo; niko tayari kuteseka mpaka kufikia ndoto hii kwa sababu; .................................... hapo sasa tiririka kwa kina KWA NINI YAKO, kama ni zaidi ya moja orodhesha kwa nini zote.

Ni muhimu unitumie KWA NINI YAKO kwani nitakuwa naitumia mara kwa mara kukukumbusha urudi kwenye njia kuu.

Kumbuka safari hii tunakwenda kwa angalau miaka kumi, haitakuwa rahisi, lazima kila aina ya silaha uwe nazo, za kukuzuia usirudi nyuma.

Hivyo shirikisha KWA NINI YAKO na nitaitumia kukusaidia usiishie njiani.

## MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii, karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021